

Maswali

1. Mbona Yesu aliponya watu?
2. Tunasoma kwa injili kwamba Yesu aliponya watu wangapi?
3. Bartimayo na rafiki wake walikuwa wakiombea wapi?
4. Nani alikuwa akienda Yeriko?
5. Bartimayo na rafiki wake walifanya nini Yesu alipokuwa akikaribia?
6. Kuita Yesu hakukuwa kwa kawaida namna gani?
7. Mwanzoni watu waliambia Bartimayo na rafiki wake wafanye nini?
8. Yesu alisema nini ifanyike?
9. Yesu alifanya nini kuwaponya?
10. Bartimayo na rafiki wake walifanya nini baadaye?

Majibu

1. Kuonyesha kwamba yeye ni Mwana wa Mungu.
2. Wanne
3. Kando ya barabara inayoelekea Yeriko.
4. Yesu.
5. Walipasa sauti wakisema, “Tuhurumie Mwana wa Daudi.”
6. Haikukuwa kawaida kuita Yesu, “Mwana wa Daudi.”
7. Waliwambia wanyamaze.
8. Aliwaamrisha wawalete Bartimayo na rafiki wake.
9. Yesu aligusa macho yao.
10. Walimfuata Yesu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 2

39 Kufumbua kipofu macho

Marejeo

Mathayo 20:29—34

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yesu anauwezo wa kipekee wa kuponya.

Maneno maalum

1. Macho + kutoona vizuri + upofu usioponywa + miujiza minne
2. Bartimayo + Yeriko + mwingine + hakuna tumaini
3. Sauti tofauti + Yesu anakuja + pasa sauti
4. Nyamaza + Yesu alisimama + furahia
5. Leta + swali + guza
6. Muujiza + furaha + akafuata

39.1 Macho yetu ni ya ajabu. Siku hizi kuna njia nyingi za kusaidia wasiona vizuri – wengi huvaa miwani. Lakini kuna wengine walio vipofu kabisa, na ni vigumu kuonywa. Yesu Kristo alipokuwa akihubiria watu, alionyesha kitambulisho cha kipekee kwa kufanya miujiza nyingi. Tunaambiwa kwa Biblia kwamba alifanya miujiza minne.

39.2 Siku moja Bartimayo alikuwa amekaa kando ya barabara iendayo Yeriko. Alikaa huko kila siku. Hapo pahali palikuwa na shuguli nyingi. Bartimayo hakukuwa na kazi yoyote hapo lakini kwa sababu alikuwa kipofu alikaa hapo akiomba ili apate chakula.

Mathayo anatwambia kulikuwa na kipofu mwingine lakini hatujaambiwa jina lake. Wote wawili walikuwa wameambiwa juu ya Yesu aliyekuwa akiponya watu wagonjwa. Walijua Yesu alizungumzia juu ya Ufalme na upendo wa Mungu. Siku hiyo Yesu alikuwa anaenda Yeriko lakini Bartimayo na rafiki yake hawakuthania atawaona au kupita walikokuwa.

39.3 Bunde si bunde wakasikia sauti karibu nao. Sauti za gari la miguu mbili na kwatu za farasi zilikuwako na zikanyamaza lakini bado kulikuwa na kelele za watu. Vipofu waliuliza watu kwamba nini ilikuwa ikiendelea. Waliambiwa, “Yesu anakuja huku.” Walifurahi sana. Wakasikiliza hizo sauti zilizokuwa zikiwakaribia. Bartimayo aliamua hivi, kufanya Yesu atambue kwamba ako hapo lazima apase sauti ya juu kuliko watu wengine wote. Alipofahamu Yesu alikuwa karibu naye, alipiga kelele na kusema, “Tuhurumie sisi mwana wa Daudi. Tuhurumie sisi.”



39.4 Watu waliokuwa karibu na Bartimayo hawakufurahia. Wakamwambia, “Bartimayo nyamaza. Yesu hataki kujishugulisha na wewe.” Lakini alipasa sauti tena, juu zaidi, “Mwana wa Daudi nihurumie.” Yesu alimsikia na akasimama. Alifurahi alipoitwa mwana wa Daudi. Makuhani hawakutaka kumuita hivyo ingawaje walijua yeye ni mwana wa Maria kutoka kwa uzao wa Daudi.

39.5 Kwa upole Yesu aliamrisha, “Leta hao watu kwangu.” Mtu mmoja kwa kikundi aliwaambia, “Anataka muende huko mbele, musiogope.” Umati wote ulinyamaza tulii. Baadhi yao waliwaongoza wale vipofu hadi mbele alikokuwa Yesu. Bartimayo alifurahi aliposikia swali la Yesu, “Unataka nikufanyie nini?” Bartimayo alijibu, “Bwana fungua macho yetu tupate kuona.” Yesu aligusa macho yao na kusema, “Enda zenu, imani yenu imemponya.”

39.6 Papo hapo walianza KUONA. Kitu cha kwanza kuona ilikuwa uso mpole wa Yesu. Baadaye waliona kikundi cha watu wengi na ukuta wa mji. Lazima walijazwa na furaha kuu. Biblia inatwambia baada ya hayo walifuata Yesu.

